# NINAKUABUDU MUNGU WANGU
## (Adoro Te Devote)

***Traditional***
***Harmony: Alex Rwelamira***




**2. Mafahamu yangu yadanganya, yanapokuona na kugusa,**
**Namsadiki Yesu hadanganyi, yeye Mungu Mwana na ukweli..**

**3. Waficha Umungu msalabani, na ubinadamu altareni,**
**Nami naungama zote mbili, kama mwivi yule mwenye toba..**

**4. Tomas aligusa majeraha, nami nasadiki bila shaka,**
**Ewe Yesu nipe pendo lako, tumaini kwako na imani..**

**5. Umeteswa nini Bwana mwema, kwa kunipa mkate wa uzima,**
**Yesu unifiche ndani yako, ili nilionje pendo lako..**

**6. Yesu Pelikane nitazame, na kwa damu yako nitakase,**
**Tone moja ndilo linatosha, na dunia yote yaokoka..**

**7. Ndani ya mafumbo Yesu yumo, atafumbuliwa kwangu lini,**
**Nikuone Yesu uso wako, nishiriki nawe heri yako.. Amina!**